# TANGAZO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

Baraza la Mitihani la Tanzania, linapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya **Mtihani wa Kidato cha Nne** (CSEE) na **Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili** (FTNA), mwaka **2026** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Usajili wa Watahiniwa wa Kujitegemea umeanza tarehe **01/01/2026** hadi **28/02/2026**. Ada ya usajili katika kipindi hicho ni Shilingi **50,000/=** kwa **Mtihani wa Kidato cha Nne** (CSEE) na Shilingi **10,000/=** kwa **Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili** (FTNA). Aidha, watakaojisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01/03/2026** hadi **31/03/2026** watalipa Shilingi **65,000/=** kwa **Mtihani wa Kidato cha Nne** (CSEE) na Shilingi **15,000/=** kwa **Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili** (FTNA), ikiwa ni ada pamoja na faini.

2. Kabla ya kusajiliwa na Mkuu wa Kituo kwenye mtandao, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua namba rejea (**reference number**) zinazotolewa **bure** na kufanya malipo ya ada kupitia Benki kwa kutumia ‘**Control Number**’.

3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu wa hatua za kufuata katika kutengeneza ‘**Control Number**’ na kujisajili, utatolewa na Mkuu wa Kituo atakachochagua Mtahiniwa kufanyia mtihani.

4. Waombaji wote wasisitizwa kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa mara baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na:

**KATIBU MTENDAJI**